

**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam  
3 Mei 2008**

**Waliohudhuria**

Ally Athuman Jumbe  
Ally Saidi Mohamedi  
Ally Saidi Mwishehe  
Aseli Wilison  
Edgar R Paulo  
Filbert Mbecha  
Husein Hamza Hamisi  
Jumanne Idd Selemani  
Kibwana Mohammad Msiga  
Markus Weise  
Mejah Mbuya  
Mussa Alex  
Ramadhani Rajabu Nyengo  
Rashidi Saidi Karanji  
Sosthenes C Amlima

**Ofisi**

Tuliamua tupake rangi za picha za guta na baisikeli ya walemavu kwenye milango ya ofisi.

**Mambo ya hela**

Juma anabaki na Tsh 14,000 ya hela ya UWABA na hakuwepo kusema kama amepata hela ya guta ya wiki tatu. Jumanne bado hajapata Tsh 10,000 kwa ajili ya lino.

**Mradi wa Usalama Barabarani - Wamba Memorial Fund**

Juma na Markus walienda benki NMB kuangalia kama hela imekuja na waliambiwa haijafika nchini. Waliambiwa kuchecki benki gani ya kati kati ilitumikwa ili NMB wanaweza kuchecki hela ipo wapi. Tuliamua tuwasiliane na Wamba Memorial Fund kujua hela imeenda benki gani kati kati.

Juma na Markus walienda Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) na HUWATA kama ilivyokubalikwa wiki jana. NIT na HUWATA wote watapenda sana kushirikiana nasi katika mradi huu na walipanga kuwa na mkutano ijumaa tarehe 2 Mei lakini tarehe haikufaa kwa kila mtu basi tutakutana nao wiki ijayo.

Elaine alimpigia simu mwalimu mkuu wa shule Mbondole na alisema ni kweli wanafunzi wengi wanaenda shuleni na baisikeli. Tulikubali wanachama wa UWABA tuwatembelee kuangalia vipi tunaweza kushirikiana. Wanachama walipendekeza tupate maandishi wa habari kuenda nasi kuonyesha kazi UWABA tunayofanya.

**Traffic police**

Juma na Markus walitembelea Traffic police na walipewa namba ya simu ya Bwana Belle ili tupange mkutano wiki ijayo.

**Mwanachama mpya**

Edgar R. Paulo amejiunga UWABA.

**Morogoro Road na TANROADS**

Juma na Markus walienda TANROADS kufuatilia na waliambiwa warudi ijumaa tarehe 2 Mei. Wakati wa wiki, tuliona kwamba TANROADS wamesharekebisha shida za vifereji maeneo ya jangwani basi TANROADS walipiga simu kusema hakuna haja ya kurudi ijumaa tena.

**Helmeti**

Mejah alisema kwamba ana helmeti 5 yupo tayari kutoa kama mchango kwa UWABA. Moja tutampa Mussa Alex, mwanachama mpya, na zingine zitaenda kwa wanachama ambao hawakupata siku la uzinduzi wa ofisi.

**Redio**

Paulo hakuwepo mkutano lakini alituma taarifa kwamba aliwasiliana na stesheni ya redio moja ili tutangaze masuala ya baisikeli. Mejah alipendekeza Radio One wana kipindi kila ijumaa kuhusu mambo ya mazingira na hii itafaa kutoa ujumbe wa UWABA. Mejah anamfahamu senior presenter Bwana Johny Nyaisanga na atawasiliana naye kuhusu kupata nafasi kwa UWABA kwenye kipindi hiki.